# Mtandao wa Kuzuia Ukatili wa Kijinsia Siku 16 za Kampeni: **Muongozo wa Matamasha: Maonyesho katika Jamii**

## Utangulizi

Siku 16 za Harakati za kampeni kikanda za mwaka huu; Wanachama wa mtandao wa kuzuia ukatili wa kijinsia katika kanda watashawishi, watahamasisha na kuwapa changamoto viongozi ili watambue Ukatili Dhidi ya Wanawake kuwa ni ukiukwaji wa haki za binadamu na kikwazo kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Tunatoa wito kwa viongozi kulaani hadharani Ukatili Dhidi ya Wanawake, na kutenga rasilimali zinazohitajika ili kuzuia na kukabiliana nao.

Tamasha ni sehemu muhimu ya kuhamasisha uongozi na jamii kuchukua hatua. Kuna nguvu katika wingi wa watu, wanachama wa mtandao wa kuzuia ukatili wa kijinsia wanahamasishwa kuandaa maonyesho katika jamii. Hili ni tukio la umma kuhamasisha jamii kuomba viongozi wao kutumia sauti zao kuchukua hatua za kukomesha Ukatili Dhidi ya Wanawake sasa. Zaidi ya hayo, pia ni fursa kwa viongozi kulaani Ukatili Dhidi ya Wanawake na kuboresha ahadi zao za kuchukua hatua za kukomesha Ukatili Dhidi ya Wanawake

Mwongozo huu mfupi unatoa baadhi ya mawazo ya kujiandaa na kuandaa maonyesho katika jamii. Tukio hili litahitaji maandalizi kwa kufanya kazi kwa karibu na asasi nyingine, wanajamii na viongozi wa aina zote – wataalamu wa serikali, viongozi waliochaguliwa, na viongozi wa dini na kimila. Unaweza kuunda 'Kamati ya maonyesho katika jamii' kuchukua jukumu la kuandaa na kuwa wenyeji wa maonyesho katika jamii. Kamati ya maonyesho katika jamii itakuwa na wajumbe walio na ari na wanaoaminiwa na jamii, wafanyakazi wako, asasi mnazoshirikiana nazo, na wanao waunga mkono ndani ya uongozi.

## Kuandaa maonyesho katika Jamii

Ufunguo wa mafanikio ya maonyesho katika jamii, ni kuandaa vizuri kwa makini na mapema. Ni matumaini yetu vidokezo hapo chini vitakuwa muhimu katika kukusaidia kupanga na kuandaa tukio lenye mafanikio.

### Hatua ya 1: Unda kamati ya maonyesho katika jamii na panga tukio

Kamati ya maonyesho katika jamii ina majukumu mengi katika kuandaa tukio hilo. Miongoni mwa shughuli zao ni kuhamasisha jamii, na kushawishi uongozi kulaani hadharani Ukatili Dhidi ya Wanawake na Wasichana. Baada ya kampeni, Kamati ya maonyesho katika jamii itakuwa na jukumu la kufuatilia ahadi zote zilizotolewa na viongozi wakati wa kipindi cha kampeni kwa kupanga na kuendesha mikutano ya wazi na ndani. Kamati ya maonyesho katika jamii inaweza kuundwa na wafanyakazi wa asasi yako, wafanyakazi wa asasi mnazoshirikiana nazo, wanao waunga mkono / machampioni kutoka ndani ya uongozi yaani, wataalamu, viongozi wa kisiasa, viongozi wa dini, viongozi wa kimila na watu wanaoheshimika katika jamii.

1. Andaa kipindi cha majadiliano (ikiwezekana ni vizuri iwe kabla ya kampeni kuanza yaani, kabla ya Novemba 10, 2015) kuwakaribisha watajwa hapo juu ambao ungependa waunde kamati ya maonyesho katika jamii. Ndani ya kikao hiki tumia maswali yafuatayo kama mwongozo:

    - Jadili kauli mbiu, dhumuni na malengo ya siku 16 za kampeni kikanda mwaka huu? (tumia mawazo katika barua ambatanisho ya kifurushi cha kuchukua hatua na utetezi)
    - Kwa kutumia karatasi kazi hii (ambayo utakuwa umeisha ikamilisha katika hatua hii) kubalianeni ni masuala gani maalumu ambayo mngependa viongozi wenu kuyashughulikia hasa yale yanayohusiana na malengo makuu ya kampeni za kikanda?
    - Jadili kuhamasisha jamii namna ya kuwabana viongozi wawajibike kwenye kampeni tajwa kupitia kwenye shughili za maonyesho katika jamii. Kitu hicho kitafanana je? Ni shughuli za aina gani utakazoweza kuzifanya (angalia hapo chini kwa baadhi ya mawazo?) Ni aina gani ya ahadi ambazo unatarajia kuzipata kutoka kwa viongozi gani hasa?
    - Ni utaalamu gani, kitu anachopendelea, uzoefu au ujuzi ambao kila mmoja katika kundi anaweza kuchangia?
    - Ni viongozi gani maarufu ambao tungependa wawepo kwenye maonyesho katika jamii na ahadi gani ambazo wanaweza kuzitoa?
    - Ni nani kati ya wajumbe walio kwenye timu atawafuata viongozi mbalimbali na kuwakaribisha katika tukio lakini pia kuwaandaa kwa ajili ya ahadi ambazo mnazitarajia kutoka kwao katika tukio hili?
    - Kubalianeni juu ya uhalisia katika utekelezaji: Ni lini maonyesho yatafanyika? Yatafanyika wapi? Ni nani watashiriki?

    Sasa, tumia taarifa kutoka kwenye majadiliano ya hapo juu ili kuamua nini kitakacho fanyika katika maonyesho katika Jamii. Shughuli zinazopendekezwa zinaweza kujumuisha yafuatayo;

    **Uwekaji mabango:** Bandika mabango juu ya ukuta, miti na kila mahali. Kuwa na wanaharakati wa jamii / wafanyakazi wawezesha majadiliano kwa kutumia mwongozo wa majadiliano. Haya yanaweza kufanyika wakati hakuna hotuba zinazoendelea ili wasihamishe mawazo ya washiriki kutoka kwenye jukwaa kuu.

    **Nafasi ya kliniki:** Omba kliniki ya eneo hilo kutayarisha kitengo cha ushauri nasaha na upimaji wa hiari wakati wa maonyesho katika jamii.

    **Michoro katika jamii:** Tafuta ukuta au tumia vipande vikubwa vya vitambaa kwaajili ya michoro katika jamii. Wakati hakuna hotuba zinazoendelea wanajamii wanaweza kuonyeshwa ujumbe unaohusiana na mahitaji ya kampeni. Hamasisha jamii kuwa wabunifu wa kutoa maoni yao juu ya jinsi ya kuzuia na kukabiliana na Ukatili Dhidi ya Wanawake na Wasichana.

**Jukwaa kuu:** Ambapo watu mbalimbali watatoa hotuba na kuwahutubia jamii. Hii ni pamoja na mtu kutoka kwenye asasi yako ataeleza mambo muhimu ya masuala yanayohusu kampeni (ukubwa wa tatizo la Ukatili Dhidi ya Wanawake na Wasichana na athari zake kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi katika nchi / jamii), mtu kutoka sekta ya utaoji huduma yaani afya, polisi, mahakama ataongea kuhusu huduma zipi zinapatikana katika jamii, mtu kutoka kwenye jamii ataainisha mapungufu yaliyopo, kiongozi wa asasi yako ataainisha sera / mapungufu ya mpango wa maendeleo ya jamii na kutoa wito kwa viongozi kulaani hadharani Ukatili Dhidi ya Wanawake na Wasichana, kuweka mipango mkakati madhubuti ya kuzuia na kukabiliana na Ukatili Dhidi ya Wanawake na Wasichana, kuweka mfumo wa Uratibu unaohusisha sekta mbalimbali, na mgawanyo wa bajeti ya kutosha kwa ajili ya utekelezaji wa mpango mkakati. Hatimaye hotuba kutoka kwa viongozi mbalimbali maarufu za kulaani Ukatili Dhidi ya Wanawake na kuweka dhamira kuhusiana na mahitaji ya kampeni /malengo, tunashauri kumuelekeza kila msemaji kufupisha hotuba yake kwa takriban dakika 15 kila mmoja.

**Mdahalo wa wazi:** Weka kipaza sauti na kundi dogo walioka kwenye viti ambapo wanajamii wanaweza kutoa maoni yao na kuhoji uongozi kwenye jukwaa. Pata washiriki miongoni mwa wafanyakazi kuwezesha hilo, toa dakika 3 (tu )kwa kila mtu kwenye jukwaa kuchangia mawazo yao juu ya unyanysaji, na jinsi gani wangependa viongozi wao na jamii kuchukua hatua.

**Shughuli nyingine:** Fanya maonyesho yenye kuelimisha, kuvutia na kufurahisha kwa kila mtu katika jamii. Andaa mchezo wa kuigiza, muziki wa bendi, michezo kwa watoto. Zaidi ya hayo, chagua watu 3-5 kutoka katika Kamati ya maonyesho katika jamii kutoa stika tano / utepe / bangili ya mkononi kwa watu watano kutoka kwa watazamaji, na anza majadiliano kuhusu Ukatili Dhidi ya Wanawake. Kundi jingine la watu kutoka Kamati ya maonyesho Katika jamii linaweza kufanya majadiliano ya kushitukiza ambayo hayakuandaliwa na vikundi vidogo vya watu kutumia mabango na muongozo wa maswali yalio kwenye mabango.

2. Kamati ya maonyesho katika jamii inahamasishwa kukaribisha na kutembelea viongozi ambao wanaona wataweza kuleta mabadiliko ambayo kundi linataraji kabla ya tukio hilo. Wakati wa ziara hii viongozi wanaweza kufahamishwa ni shughuli gani zimepangwa na ahadi ambazo kundi lina matumaini ya kufanikisha kuhusiana na mahitaji ya kampeni. Weka watu tofauti katika kundi wenye jukumu la kualika viongozi mbalimbali.
3. Tengeneza Vidokezo vya Kuzungumzia / hotuba kwa wasemaji mbalimbali katika tukio hilo.
4. Kubalianeni ndani ya kundi nani ambaye atahamasisha na kukaribisha wanajamii kwenye maonyesho katika jamii, nani atandaa kliniki ya ushauri nasaha na upimaji wa hiari, nani atahamasisha vyombo vya habari, nani ataandaa muongozo wa majadiliano kwa kutumia mabango nk
5. Unapoandaa mpango na kupanga kazi kumbuka kujumuisha tarehe maalum kwaajili ya ufuatiliaji pamoja na wenzako.

## Hatua ya 2: kuhamasisha maonyesho katika jamii

1. Kama timu (kamati ya maonyesho katika jamii), chagua sehemu inayofahamika vizuri,iliyo katikati ya mji, inayowezana kufikika na umma na inayoweza kufanyika tukio na tafuta kibali kutoka kwa mamlaka husika.
2. Karibisha makundi mbalimbali ya viongozi (wataalamu, viongozi waliochaguliwa, viongozi wa dini, na viongozi wa kimila) kama ilivojadiliwa katika hatua ya 1 hapo juu

3. Tangaza sana: tuma mialiko kupitia barua pepe, ujumbe mfupi wa maandishi, na piga simu, gawa vijarida / au vipeperushi, tangaza kwenye redio, nk
4. Kumbuka kujumuisha wapi, lini, nini na nani, katika mwaliko / vipeperushi / matangazo ya redio / gari la matangazo.
5. Tengeneza vipeperushi kuwajulisha watu kuhusu tukio: ni wapi na lini litafanyika.
6. Hakikisha taarifa zinachukuliwa! Karibisha vyombo vya habari kwenye tukio - jadili vidokezo vya kuzungumzia, tayarisha mahojiano (na viongozi wakati wa tukio hilo hakikisha wanarudia ahadi zao katika mahojiano yao), na kushiriki taarifa mbadala na vyombo vya habari. Tumia mkutano na waandishi wa habari na vidokezo vya kuzungumzia kukusaidia katika majadiliano haya.
7. Hakikisha umejiandaa vya kutosha kuzungumza na vyombo vya habari. Kubalianeni ni nani atakaye jibu maswali kutoka kwenye vyombo vya habari na jadili vidokezo vya mazungumzo pamoja nao.
8. Fuatilia majukumu yote kama vile kukodisha mifumo ya vipaza sauti, kupata viti, kutafuta mgeni rasmi, kuandika hotuba yake
9. Panga kikao cha maandalizi ili kuhakikisha hotuba ziko sahihi na zinaeleweka, hamasisha watu kutoa hotuba zao wakiwa na ari.
10. Karibisha wadau kutoka taasisi husika na kumbuka kutafiti juu ya itifaki sahihi kwa wageni rasmi kutoka serikalini
11. Angalia vifaa na vyanzo vyote vya umeme, kabla ya tukio hilo.
12. Gawanya majukumu kwa siku ya tukio, kwa mfano uandikishaji, kuratibu wageni watakao toa hotuba nk. Onyesha shughuli za tukio hilo na mshereheshaji mkuu.
13. Kamati ya maonyesho katika jamii inapaswa kuandaa mkutano siku moja kabla ya tukio ili kuhakikisha kuwa maandalizi yote muhimu yapo sahihi.

## Hatua ya 3: Utekelezaji wa maonyesho katika jamii

1. Fanya mkutano na timu yenye hamasa kabla ya tukio ili kuongeza nguvu kwa vikundi vya wanaharakati wa jamii.
2. Fika mapema kwenye eneo la tukio kuandaa vifaa vyote na utaratibu wa shughuli.
3. Hakikisha mratibu mkuu wa shughuli anawasiliana na watu wote kwenye timu ili waweze kuangalia maendeleo ya shughuli.
4. Hakikisha wafanyakazi wapo kwenye maeneo yao waliopangwa kwa ajili ya kusalimiana na wageni, kufuatilia utaratibu wa shughuli, kujiandikisha na kukaribisha nk
5. Shukuru kila mtu kwa kufika.
6. Andaa sherehe ya timu baada ya tukio hilo.

## Hatua ya 4: Ufuatiliaji

1. Fanya mkutano na kamati ya maonyesho katika jamii baada ya tukio, kujadili jinsi lilivyofanyika, mambo mlio jifunza, na mambo muhimu ya kufuatilia nk
2. Pongeza kila mmoja kwenye timu, kiri na thamini mchango wa kila mtu kwenye tukio hilo.
3. Panga mkutano wa ufuatiliaji wa kamati ya maonyesho katika jamii ili kuandaa mpango mkakati wa kufuatilia ahadi zilizotolewa na viongozi katika maonyesho katika jamii.
4. Kamati ya maonyesho katika jamii ipange mikutano ya jamii ili jamii iweze kuwa na taarifa kuhusu maendeleo ya ahadi zilizotolewa

Kuwa na mtazamo chanya! **Huu ni muda wa kupaza sauti yako na kuchukua hatua ya kukomesha Ukatili Dhidi ya Wanawake!**

Fanya kazi ya kushawishi, kuhamasisha na kutoa changamoto kwa uongozi ili kukomesha Ukatili Dhidi ya Wanawake na Wasichana italeta changamoto, lakini pia inatoa fursa nyingi zitakazowezesha kufanya kazi nzuri, hamasisha jamii na jenga uwakala wao, na kukuza madai yao na matokeo.

Usisite kuwasiliana na ofisi ya uratibu kwa msaada wowote au tu kushirikisha taarifa yako. Tunakutakia mafanikio mema katika Siku 16 2013 za kushirikiana!

Tunakutakia tukio lenye mafanikio la siku 16 2015!